



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA

BARAZA LA WATAALAMU WA MAABARA



Tovuti: [www.hlpc.go.tz](http://www.hlpc.go.tz)

## TANGAZO

### KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA MAOMBI YA MITIHANI YA USAJILI

Baraza la Wataalamu wa Maabara linachukuwa nafasi hii kuwajulisha Wataalamu wote wanaotarajia kufanya maombi ya mitihani ya usajili kwa ngazi ya Shahada (Bachelor Degree) kuwa dirisha la maombi ya mitihani ya usajili litafunguliwa rasmi tarehe **22 Agosti 2022** na litafungwa tarehe **20 Oktoba 2022** saa 9:30 alasiri.

Watahiniwa wote watakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo;

1. Wataalamu wenye usajili wa awali (PRP) ambao umekwisha muda au umebakiza miezi miwili (2) na wale wa marudio (supplementary) ndio watatakiwa kufanya maombi ya mitihani.
2. Maombi ya kupata "control number" kwa ajili ya malipo yatumwe kwa njia ya ujumbe mfupi (SMS) kwenda 0734005777 yakiwa na Majina kamili, Namba ya usajili wa awali (PRP), kiasi kinacholipwa, kituo unachopenda kufanya mtihani na aina ya mtihani utakaofanya (First sit/Supplementary). Ikiwa ni marudio (supplementary) ainisha kama ni nadharia, vitendo au yote.
3. Baada ya dirisha kufungwa, orodha ya watahiniwa na vituo vyao vya mitihani vitawekwa kwenye tovuti ya Baraza ([www.hlpc.go.tz](http://www.hlpc.go.tz))
4. Vituo vya mitihani ni **KCMUCo** – Kilimanjaro, **CUHAS** - Bugando Mwanza, **MUHAS & St. Joseph** – Dar es salaam, **Amenye** – Mbeya na **UDOM** – Dodoma.
5. Wanaofanya mafunzo ya utarajali MNH watafanya mitihani katika kituo cha MUHAS na wanaofanya mafunzo ya utarajali maeneo tofauti na MNH watafanya Mitihani kituo cha ST. Joseph – Dar es salaam.

**Angalizo:** 1. Maombi haya **HAYAFANYIKI** kwenye mfumo wa baraza (HPRS) kwa Sasa, hivyo kwa msaada zaidi piga simu ya ofisi 0734005777.

2. **Maombi yatakayotumwa Baada ya terehe 20 Oktoba 2022 saa 9: 30 Alasiri HAYATAFANYIWA KAZI.**

Upatapo tangazo hili mtaarifu mwenzako.

Imetolewa na

Msajili

Baraza la Wataalamu wa Maabara